

KATIBA

YA

RENGUA VICOBA GROUP

UTANGULIZI

hii ni mali ya wanachama wa kikundi Cha Rengua vicoba group. Rengua vicoba kikundi cha kuweka na kukopa chenye Mlengo VICOBA kili-choanzishwa rasmi tarehe 12/11/2022.

Rengua vicoba group ni kikundi cha wajasiriamali waishio kata ya Mawenzi katika Manispaa ya Moshi. kilianzishwa kwa mlengo au kwa dhumuni la kuwawezesha wajasiriamali kuwasaidia katika shughuli zao za kimaendeleo na waweze kujiongezea ajira kwa mfumo wa kuweka na kukopa ili kupata mitaji.

(Village Community Bank). Mfumo huu (VICOBA) unawezesha jamii kuunganisha nguvu na rasilimali kujiletea maendeleo kwa Kupunguza umaskini wakipato na kuboresha maisha ya familia.

Rengua Vicoba group ni kikundi kisicho na ubaguzi wa aina yoyote kama vile:- rangi, siasa, kabila. Hivyo basi miiko ya kutoa mikopo na nasharti yake yanawekwa na wanachama wa VICOBA vikizingatia kumsaidia mwanakikundi na wala sio kumyonya au kukandamiza ili kunufaisha mtu yeyote au kiongozi yeyote wa kikundi au hisa-zake zitumike kunnufaisha mtu asiye katika mtandao wa vikundi hivi.

Katiba hii ni mawazo, makubaliano na mali ya Rengua Vicoba group na sio mali ya kiongozi yeyote au mtu binafsi.

Hivyo katiba hii ni muongozo wa shughuli na maamuzi mbalim-

bali ya kikundi cha Rengua Vicoba group.

Katiba hii inaweza kufanyiwa

marekebisho na-

wanakikundi wakishirikiana tna viongozi wa kikundi katika wakati wowote katika vikao halali.

Inapobidi hasa kwa malengo ya kuboresha utendaji kazi wa kikundi na kuboresha maisha ya wanachama wa Rengua vicoba group.

TAMKO RASMI:

Sisi wanakikundi cha Rengua Vicoba group tunatamka rasmi leo tumekubaliana valivoandikwa katika katiba hiki kuwa ndio katiba yetu. Hivyo tunaahidi kuifuata kama muongozo wetu katika kupitisha maamuzi na utekelezaji wa shughuli zetu za kila siku.

MWENYEKITI-----

TAREHE. -----

KATIBU -----

TAREHE -----

SEHEMLYA KWANZA

TAARIFA ZA MSINGI WA KIKUNDI

Jina la kikundi: RENGUA VICOBA GROUP.

Anwani ya kikundi I I 68 MOSHI

Kikundi kiliundwa tarehe 12/11/2022

Tarehe ya kuandikishwa kikundi-----

MADHUMUNI YA KIKUNDI

Madhununi ya kikundi ni kuwa huru, kutoa huduma ya kifedha kwa wanachama wote.

Huduma zitazotolewa kwa wanachama ili kufikia malengo yake ni: Kuweka na kukopa na biashara ndogondogo.

MAHUSIANO YA KIKUNDI NA WATOA HUDUMA ZA KIFEDHA WENGINE.

Kikundi hakitakopa katika vyanzo vingine vya fedha katika mzunguko wa

Pili wa kuweka na kukopa. Kama

watafanya hivyo kwenye mzunguko

unaofuata watafuata masharti yafuatayo:

Mkopo wa kikundi hautozidi thamani ya

fedha walizokuwa nazokwenye mzunguko

wa kwanza na wapili. Kikundi ndicho

kitakachochukua mkopo na sio

wanachana mmoja mmoja.

Kikundi watakopesha wanachama tu na si vinginevyo.

Kama kikundi kitakubaliana kukopa katika

vyanzo vingine vya mapato mkopo wao

usizidi mara tatu ya hisa walizonazo.

Kama wanachama watakopa kutoka kwenye vyanzo vingine vya fedha, kikundi ha-wataruhusu akiba za wanachama kuwekwa kama dhamana kwa usalana wa mikopo hiyo.

UANACHAMA

Umri kuanzia niaka 18 na kuendelea

Jinsia Me/Ke.

Kingine kinachowaunganisha kusaidiana

kwenye shida WAJUMBE WA KAMATI

Mwenyekiti

Katibu

mweka hazina

SEHEMU YA PILI

UONGOZI

NGAZI ZA UONGOZI NDANI YA KIKUNDI
Kutakuwa na aina mbili za uongozi wa
kikundi cha RENGUA Vicoba-Group."
Ufuatao ni uongozi ndani ya kikundi cha
RENGUA Vicoba Group.

Kamati tendaji itakuwa na viongozi ambao
ni:-Mwenyekiti wa kikundi

Katibu wa kikundi

Mtunza fedha

SEHEM! YA PILI

UONGEZI

Viongozi wenye dhamana maalum;

Mtunza nidhamu

MWENYEKITI

Kufungua, kusimania na kufunga
mikutano/vikao Kutangaza mapato,
mkopo na marejesho

Kupokea wageni wa kikundi na kutoa
maelekezo. Mwakilishi wa kikundi kwenye
mialiko mbalimbali.

MTUNZA NIDHAMU

Kusimamia utekeleza wva sheria

Kukusanya adhabu / faini

Kumsindikiza mweka hazina kwenda bank

Kumshauri mwenyekiti wa kikundi

KATIBU

Kuandika kumbukumbu

Kuandika muhtasari ya mikutano na vikao
vya kikundi Kumsaidia mwenyekiti katika
kazi zake

Kuita namba za wanakikundi wakati wa
kununua hisa Kusimamia michango
mbalimbali

Kuandaa taarifa ya tathmini ya mzunguko

Ni mtia sahihi namba moja katika akaunti
ya kikundi.

MWEKA HAZINA

Kutunza bagi au sanduku/kasick na mali
nyingine za kikundi Kuleta taarifa ya
fedha.

Kukagua fedha za hisa, marejesho na
michango

Kumsaidia katibu

Msimamizi mkuu katika akaunti ya

kikundi/kupeleka pesa bank

UKOMO WA UCHAGUZI WA VIONGOZI

Ukomo wa viongozi unategemea utendaji
kazi na wanachama kuridhika nao.

Viongozi wa kikundi watachaguliwa kwa
kupigiwa kura za siri.

Au kwajinsi wanachama

watakavyokubaliana

MIKUTANO YA KIKUNDI

Kutakuwa na mikutano ya aina tatu ya

kikundi cha Rengua Vicoba Group nayo

ni-Mkutano wa mwezi , mkutano

maalum/dharura na mkutano wa mwisho

wa kufunga mwaka.

UTARATIBU WA UCHAGUZI

Uchaguzi lazima ufanyike mwamzoni mwa mwaka

Idadi ya chini ya wagombea kwa nafasi moja ni 2

Mwanachama anaweza kurudi kuchaguliwa uongozi. Chini ya wanachama wanaoweza kuendesha uchaguzi ni $\frac{1}{2}$ ya wanachama wote.

Uchaguzi utakuwa ni kura za siri

Mgombea ni lazima apendekezwe na wanachama wenzake kabla ya kugombea
KUONDOLEWA MADARAKANI KWA WAJUMBE WA KAMATI YA UONGOZI KABLA YA UCHAGUZI.

Kiongozi anaweza kuondolewa madarakani na wanachama wakati wowote Kiongozi ni lazima akubali kujiuzulu endapo wanachama hawamkubali Kujaza nafasi ya aliyeondolewa ni lazima utaratibu wa uchaguzi ufuatwe.

MIKUTANO

Kikundi kitakutana kila wiki kununua hisa Hisa zitanunuliwa katika kila mkutano, lakini utoaji na urejeshaji wa mikopo utafanyika kila mwezi kulingana na mda uliochukua mkopo.

KUACHA UANACHAMA NA KUFUKUZWA

Kama mwanachama anaacha uanachama kabla ya mzunguko kuisha atarudishiwa fedha yake ya hisa baada ya makato ya mkopo unaodaiwa na fedha nyingine anazodaiwa.

Sababu za mwanachama kufukuzwa kikundi:-

Kutoa siri za kikundi.-

Kutowekwa hisa mara nne kwa wiki na nidhamu mbaya katika kikundi Pamoja na mengine kama hayo yanayohatarisha usalama wa kikundi.

FAINI

Jedwali lifuatalo linaonesha mtiririko wa adhabu kwa kila kosa katika kikundi.

KOSA

Kutohudhuria mkutano kwa sababu binafsi sh 5,000

Kuchelewa kufika kwenye mkutano sh 1;000

Kuchelewa kurejesha mkopo kwa mda ni

asilimia 10 ya rejesho husika Kutoleta
hisa na dharura sh 2,000
Kucheleweshha hisa na dharura sh 1,000
Kudharau maamuzi ya kikundi sh 2000
Kuonyesha dharau kwa viongozi au
wanachama sh 10,000
Kuacha uanachama kwa sababu zisizo na
msingi sh 50,000
Kulala kwenye mkutano sh 1000

VIWANGO VYWA KUSAIDIANA

UGONJWA: mwanachama akiugua na kulazwa ndani ya siku tatu au ugonjwa utakaomfanya akae nyumbani kila mwanachama atachangia sh 10,000 na kikundi kitatoa sh 50,000 kwenye mfuko wa dharura.

Endapo mwanachama atauguliwa na mtoto au mke wanaoishi naye nyumbani kila mwanachama atachangia sh 5,000 Mwanachama akiugua ugonjwa wa mda mrefu kila wiki wanachama watachangia sh 2000/;

MSIBA:

Endapo mwanachama atafariki kila mwanachama atachangia sh 20,000 na mfuko wa dharura itatolewa sh 100,000. Endapo mwanachama atafiwa na mtoto au mke wanaoishi naye nyumbani kila mwanachama atachangia sh 10,000.

VIWANGO VYWA MIKOPO:

Kuanzia sh 1000 hadi 100,000 UKOMO mwezi mmoja

Kuanzia sh 110,000 hadi 499.000

UKOMO miezi mitatu

Kuanzia sh 500,000hadi

1,500,000UKOMO miezi sita

Kuanzia sh 1;600,000 hadi 1,999;000

UKOMA miezi nane

Kuanzia 2,000,000 hadi 3;000,000

UKOMO miezi kumi na mbili

MASHARTI YA MKOPAJI

Kujaza fom.

Paspoti mbili ya mdhamini na mkopaji

Kopi ya kitambulisho cha mkopaji na mdhamini.

MAREKEBISHO YA KATIBA

Nusu ya wanachama lazima wakubali kurekcbisha katiba

Mwanachama yeyote anaweza kutoa pendekezo la kurekebisha katiba.

1. AKIBA

SEHEMU YA TATU

HUDUMA ZITOLEWAZO

Mwanachama anaweza kununua hisa 1 na kuendelea katika mkutano mmoja. Thamani ya hisa moja itakuwa 5000/ dharura 1000

Wanachama wanaweza kukubaliana na kuchanga kianzio kwa kima sawa kwa wote katika mzunguko unaoanza ili kuharakisha ukuaji wa mtaji wa kukopeshana.

MIKOPO

Kima cha chini mwanachama anaweza kukopa ni mara tatu ya hisa zake.

Muda mrefu wa mkopo ni miezi 12, Mwanachama ni lazima alipe mkopo kabla hajachukua mwingine

Kama mwanachama akifariki akiwa na mkopo, wanachama watafanya ifuatavyo:- Watapiga hesabu za hisa zake watazikata deni litakalobaki atalipa mdhamini wake kwa kushirikiana na familia ya aliyekufa.: Mkopo utatolewa kwa dhumuni la BIASHARA tu.

Mkopaji akifukuzwa uanachama na ana deni mdhamini atahakikisha deni linalipwa kwa mda walioweka wanachama.

Kurenw mkopo ni mara moja tu baada ya hapo hatua zitakazopendwekezwa na wanachama zitachukuliwa.

Mwanachama atafanya marejesho kila mwezi kulingana na mda wa mkopo wake akishindwa atapaswa kulipa faini asilimia 10 ya rejesho lake.

MFUKO WA DHARURA:

Mfuko wa dharura ni wa kutoa msaada kwa wagonjwa na vifo kulingana na makubaliano ya wanachama pamoja na matumizi ya kikundi.

Kila mwanachama mpya atapaswa kulipa tangia mwanzo wa mzunguko ulipoanza.

Kuchangia mfuko wa dharura kila wiki utakuwa Tsh 1000/=

Mwanachama akiumwa na kulazwa ndani ya siku tatu mfuko utachangia sh 50,000/;